



JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA EKIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
CHUO KIKUU CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI MUHIMBILI
(MUHAS)



P.O. Box 65001
Dar es Salaam.

Tel. G/Line: +255-22-2150302/6
Telefax: +255-22-2150465
E-mail: vc@muhas.ac.tz

Ref. No. CA. 455/524/27

02 Juni, 2026

TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI

Makamu Mkuu wa Chuo, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) anapenda kuwataarifu Waombaji Kazi wote walioomba kazi nafasi ya “Dental Surgeon II”, Health Laboratory Technician II and Radiographic Technician II” kuwa usaili wa mahojiano unatarajiwa kuendeshwa tarehe 10/06/2026 hatimaye kuwapangia majukumu waombaji kazi watakaofaulu usaili huo. Wasailiwa wanaliotwa kwenye usaili wanapaswa kuzingatia maelekezo yafuatayo: -

1. Usaili utafanyika kuanzia tarehe kama ilivyooneshwa kwenye tangazo hili muda na sehemu ambapo usaili utafanyika umeainishwa kwa kila Kada.
2. Kila Msailiwa anapaswa kuwa na kitambulisho kwa ajili ya utambuzi. Vitambulisho vinavyokubalika ni pamoja na: - **Kitambulisho cha Mkazi, Kitambulisho cha Mpiga kura, Kitambulisho cha kazi, Kitambulisho cha Uraia, Hati ya kusafiria, Leseni ya Udereva au barua ya utambulisho kutoka Serikali ya Mtaa/Kijiji anachotoka.**
3. Wasailiwa wanatakiwa kufika na VYETI VYAO HALISI, kuanzia cheti cha kuzaliwa, kidato cha IV, VI, Astashahada, Stashahada, Stashahada ya Juu, Shahada na kuendelea kutegemeana na sifa za nafasi husika.
4. Wasailiwa watakaowasilisha ‘Testimonials, Provisional Results, Statement of results’, hati za matokeo za kidato cha IV na VI (‘form IV and form VI results slips’) **HAVITAKUBALIWA NA HAWATARUHUSIWA KUENDELEA NA USAILI.**
5. Kwa kada ambazo wanatakiwa kusajiliwa na Bodi za Kitaaluma wanapaswa kuja na vyeti vyao Halisi vya Usajili pamoja na Leseni za kufanyia kazi
6. Kila msailiwa atajigharamia kwa Chakula, Usafiri na Malazi. Aidha kila msailiwa anapaswa kuhudhuria usaili akiwa na **mavazi nadhifu na yenye staha** kulingana na Waraka wa mavazi.
7. Kwa wasailiwa waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe Vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (kama TCU, NACTVET au NECTA).
8. Wasailiwa ambao hawajaona majina yao kwenye tangazo hili watambue kuwa hawakukidhi sifa/vigezo na mahitaji ya nafasi walizoomba.
9. Wasailiwa ambao majina yao yanatofautiana katika nyaraka zao wanapaswa kuwasilisha Hati ya Kiapo cha Kubadili Jina (**Deed Poll**) iliyosajiliwa na **Wizara ya Ardhi.**

RATIBA YA USAILI WA VITENDO NA MAHOJIANO

Na.	MWAJIRI	KADA	TAREHE YA USAILI WA VITENDO	TAREHE YA USAILI WA MAHOJIANO	MAHALI
1	CHUO KIKUU CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI MUHIMBILI (MUHAS)	"Dental Surgeon II"	Hakuna	10.06.2026 01:00:00 (Asubuhi)	SCHOOL DENTISTRY (MUHAS)
		"Health Laboratory Technician II"	Tarehe 10.06.2026 saa 01:00:00 (Asubuhi)	10.06.2026 06:00:00 (Mchana)	
		"Radiographic Technician II"	Hakuna	10.06.2026 01:00:00 (Asubuhi)	

MWAJIRI: MUHAS

KADA: "DENTAL SURGEON II"

TAREHE YA USAILI WA MAHOJIANO: 10:06:2026 saa 01:00:00 (Asubuhi)

MAHALI: SCHOOL OF DENTISTRY (MUHAS)

NA	JINA LA MWOMBAJI
1	Daniel Kweka

MWAJIRI: MUHAS

KADA: "HEALTH LABORATORY TECHNICIAN II"

TAREHE YA USAILI WA VITENDO: 10:06:2026 saa 01:00:00 (Asubuhi)

TAREHE YA USAILI WA MAHOJIANO: 10:06:2026 saa 01:00:00 (Asubuhi)

MAHALI: SCHOOL OF DENTISTRY (MUHAS)

NA	JINA LA MWOMBAJI
1	Waridi Masoud Yassin
2	Kataga Albert Modest
3	Azori Abinery Max
4	Ashraf Yusuph

MWAJIRI: MUHAS

KADA: "RADIOGRAPHIC TECHNICIAN II"

TAREHE YA USAILI WA MAHOJIANO: 10:06:2026 saa 01:00:00 (Asubuhi)

MAHALI: SCHOOL OF DENTISTRY (MUHAS)

NA	JINA LA MWOMBAJI
1	John Eliud Shao
2	Laurence D. Mtwanzi
3	JUMA RAHIM USANGA
4	Felician Chatamanta Komango
5	JulianaJohn Shirima
6	Laizer Ezekiel Oloidi

IMETOLEWA NA;

**MAKAMU MKUU WA CHUO
CHUO KIKUU CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI MUHIMBILI**